## Jinsi ya kushiriki

SHIRIKI KATIKA TAFITI ZETU

Kama utapenda kushiriki katika utafiti wetu , tafadhali tuandikie kwa barua pepe: UPSIDES@uni-ulm.de

KUTANA NA WATAFITI

Pata timu ya kila eneo la utafiti https://www.upsides.org/consortium/ na utuandikie ili kujua zaidi!

## Wasiliana nasi

### Tembelea ukurasa wetu

Je ungependa kujua sisi ni kina nani na tunafanya nini? Tanzama tovuti yetu!

https://www.upsides.org

MTANDAO WA KIJAMII

Pata taarifa za hadi leo kupitia Twitter:@UpsidesProject

Kiandikishe katika jarida letu kwa kuwasiliana na UPSIDES@uni-ulm.de


TAARIFA ZA MAWASILIANO

Ifakara Health Institute

+255683105670

Mr. Donat Shamba

dshamba@ihi.or.tz


JARIDA LIFUATALO: #06

→ Sasisha juu ya hali ya Covid-19 katika maeneo ya utafiti ya mradi wa UPSIDES
→Mahojiano na Dr. Galia Moran (Israel)

Tuma taarifa zako kwa UPSIDES@uni-ulm.de ili uzione kwenye jarida lifuatalo!

# UPSIDES

# JARIDA

#05
Juni
2020

## #05-MADA

Madhara ya COVID-19: Mahojiano na Lisa Wenzel na Dr. Bernd Puschner

Ni jinsi gani maeneo ya utafiti yanawasaidia wawezeshaji rika wa UPSIDES katika kipindi cha janga la COVID-19?


UPSIDES imepokea ufadhili kutoka European Union's Horizon 2020 research and innovation programme chini ya makubaliano no. No 779263. Jarida hili linaonyesha mtazamo wa waandishi tu. Tume haihusiki na taarifa zilizopo..


www.upsides.org

Ulimwenguni kote, janga la Corona limebadili maisha na mipango ya mradi wa UPSIDES imebidi izingatiwe tena. Kwahiyo tumebadili mada za jarida hili (tofauti na tangazo lililokuwa kwenye jarida #4). Sasa tutatoa ripoti juu ya athari za janga la Corona kwenye mradi wa UPSIDES.

## Muitikio wa COVID-19 kwenye maeneo ya utafiti ya mradi wa UPSIDES

Kwa kuzingatia janga la Covid-19, mabadiliko ya muda ila ya msingi ilibidi yafanyike kwenye maeneo ya utafiti ya mradi wa UPSIDES kuhakikisha usalama wa wawezeshaji rika na washiriki wa utafiti katika kila eneo la utafiti kulingana na hatua zilizochukuliwa na serikali au taasisi. Mpango wa usumamizi wa majanga uliandaliwa ili kusimamia hatari katika kila eneo la utafiti.

Hali inasimamiwa kila wakati ili kuweka taarifa za mabadiliko katika kila eneo la utafiti. Maeneo mengi ya utafiti yaliona kwamba kuwaomba wawezeshaji rika kufanyia kazi nyumbani kwa ajili ya usalama wao lilikuwa jambo la msaada. Ingawa, ukosefu wa simu, mtandao vimekuwa ni vikwazo katika ufuatiliaji na mawasiliano kati ya wawezeshaji rika na washiriki wa utafiti.

## Mahojiano na Lisa Wenzel (research worker) and Dr. Bernd Puschner (UPSIDES coordinator)

*Q: Unaweza kutueleza kuhusu mchakato wa kuandaa muongozo wa Covid-19?*

Swali la kwanza tulilojiuliza ni jinsi gani utafiti unaweza kuendelea katika mazingira yaliyopo na jinis gani unaweza kutekelezwa, Katika kufanya hivyo tuliendelea kufuatilia vizuizi vya COVID-1 ambavyo vinaendelea kutumika katika kile eneo la utafiti. Ufuatiliaji huu wa COVID-19 uliongozwa na mwenzetu Ramona Hiltensperger ambaye alijadili suala hili kwa kufanya mawasiliano mbalimbali na maeneo ya utafiti katika wiki zizizopita, mbali na utaratibu wa kawaida wa mawasiliano ambao ulikuwepo. Kwakuwa usalama wa wote wanaohusika ni muhimu sana kwetu, tuliainisha hatua madhubuti za kiusalama zitakazotumika katika kuendeleza utafiti wa UPSIDES.

*Q: Kulikuwa na changamoto zipi katika kuandaa huo muongozo?*

Kwasababu ya kutofautiana kwa janga la COVID-19 katika kila eneo la utafiti, changamoto mojawapo ni kuandaa muongozo mmoja ambao utatumika katika kila eneo la utafiti..

Mkakati wa jumla wa kuanza upya ni kuendelea na utafiti wa UPSIDES RCT kwa kuzingatia miongozo ya kiutafiti, lakini hatua zote lazima ziendane na taratibu za eneo husika, serikali na taasisi nyingine zinazzohusika (kwa mfano hospitali,watoa huduma wengine, nk). Kwa ujumla, maandalizi ya utafiti mkuu pamoja na ushirikiano mzuri katika maeneo ya utafiti yatatusaidia kukabiliana na janga lililopo kwa njia nzuri kadri iwezekanavyo.

*Q: Ni kwa namna gani janga la Covid-19 limeathiri utafiti katika eneo lako la utafiti? Na unatabiri hii itaathiri vipi kazi za UPSIDES katika miezi ijayo?*

Tangu kusitishwa kwa shughuli za kawaida na mikusanyiko ili kukabiliana na janga la Covid-19 huduma, utafutaji wa washiriki na ukusanyaji wa takwimu katika utafiti zimesimama. Wakati huo huo juhudi mbalimbali zilifanyika kuzuia upotevu wa washiriki na kuhakikisha afya njema kwa wafanyakazi na washiriki katika kipindi hiki. Katika siku zijazo kila mmoja atakuwa makini zaidi kuliko ilivyokuwa ili kuhakikisha usalama kazini.

## Ni jinsi gani maeneo ya utafiti yanavyowasaidia wawezeshaji rika katika kipindi cha janga la Covid-19?

Katika kipindi hiki cha janga la Covid-19 timu za watafiti wa UPSIDES zinachukua hatua zote kuhakikisha usalama na afya njema kwa wawezeshaji rika, washiriki wa utafiti na jamii. Wakati baadhi yetu tumelazimika kufanya kazi kutokea nyumbani, tumeendelea kusisitiza katika mshikamano na matumaini zikiwa ni baadhi ya kanuni muhimu za uwezeshaji rika. Timu yetu wamekuwa wabunifu katika kuanzisha mawasiliano kwa njia ya mtandao na vikao kwa njia ya video kati ya watafiti na wawezeshaji rika licha ya changamoto zilizopo. Kwa kuzingatia maadili washiriki wote wa utafiti walitaarifiwa kuhusiana na kusimama kwa utafiti. Vituo vya utafiti vilivyopo Ujerumani vya Hamburg na Ulm wanawashirikisha wasaidizi rika katika uandaaji wa makala ya kitaaluma kuwashirikisha wengine uzoefu wao. Katika njia ya kutoa msaada kwa vitendo katika kipindi hiki kigumu katika kituo chetu cha Butabika imekodisha pikipiki na kupeleka dawa nyumbani kwa wawezeshaji rika.

Nchini India video za kuelimisha kuhusiana na Covid-19 na kujitunza katika kipindi cha kusitishwa kwa shughuli za kawaida zilitumwa kwa wawezeshajisaidizi rika. Kundi la mtandao wa facebook kwaajili ya wawezeshajii rika linafanya kazi kwa maeneo yote ya utafiti vyenye mtandao wa intaneti na linaweza kuwa msaada baina yao.

Wawezeshaji rika ndiyo kiini cha shughuli za utafiti wa UPSIDES. Ili kuweza kuwa na muendelezo tunahitaji muendelezo wa majadiliano kati ya wawezeshaji rika na jamii inayowazunguka. Katika jarida lifuatalo tutaangalia kwa undani ni jinsi gani meneo ya utafiti yalivyomudu utekelezaji wa shuguli za uwezeshaji rika licha ya taratibu za udhibiti wa Covid-19 katika moja ya kituo chetu cha Israeli. Jarida hilo litaangalia mchakato unaoendelea wa utatuaji wa matatizo na ubunifu katika utekelezaji wa utafiti.